

Lessoni ya 3: Manabii wa Agano la Kale

A. Nabii Yahazieli

1. Yehazieli alitoa unabii gani wakati wa shida ya kitaifa katika Yuda? 2 Mambo ya Nyakati 20:14-17
2. Mfalme Yehoshafati alitendaje kulingana na unabii wa Yahasieli? 2 Mambo ya Nyakati 20:18-20
3. Ni manabii gani wa zamani au wa sasa wa Mungu ambao watu wa Yuda wangaliwajua wakati huu? (Katikati ya karne ya 9 K.W.K.) Musa, Miriamu, Debora, Samweli, Eliya, Elisha, n.k.
4. Ni mambo gani tunayoweza kujifunza kutokana na unabii wa Yahazieli? (tazama 2 Mambo ya Nyakati 20:21-22)

B. Kazi za nabii wa Mungu

1. Ni kazi gani za nabii wa Mungu zinazofichuliwa katika wito na huduma ya nabii Samweli? 1 Samweli 3:1-10, 19-21 8:1-10
2. Ni kazi gani za nabii wa Mungu zinazofunuliwa katika wito wa Yona? Yona 1:1-3,3:1-2
3. Ni kazi gani za nabii wa Mungu zinazofunuliwa katika wito wa nabii Yereimia? Yereimia 1:4-10`
4. Ni kazi gani za nabii wa Mungu zinazofunuliwa katika huduma ya Hulda? 2 Wafalme 22:12-20
5. Tunaweza kujifunza nini kutokana na ukweli kwamba manabii walikuwa vijana na wazee, wanaume na wanawake? Yoeli 2:28-29

C. Manabii wa Mungu walikuwa watu wasio wakamilifu

1. Kama tulivyoona kutokana na hadithi ya Yona, manabii wa Mungu walikuwa watu wasio wakamilifu.
2. Yakobo 5:17-18 Yakobo alikuwa akimaanisha nini alipomwelezea nabii Eliya kama mtu "aliye na asili kama yetu"? 1 Wafalme 19:2-4)
3. Ni masimulizi gani mengine katika Agano la Kale yanayotukumbusha kwamba manabii wa Mungu walikuwa watu wasio wakamilifu? Mwanzo 9:20-21, Hesabu 12:1-10, 20:7-11, 2 Samweli 11:2-4, n.k.
4. Ni somo gani tunaweza kujifunza kwa ajili ya maisha yetu leo ikiwa Mungu anaweza kuwatumia watu wasio wakamilifu kusema kwa niaba Yake?
5. Simulia wakati ambapo Mungu alikutumia kusema kwa niaba Yake ingawa ulifahamu vizuri udhaifu na kutokamilika kwako.

D. Manabii wa kweli wa Mungu na manabii wa uwongo

1. Ni mambo gani tunayoweza kujifunza kutokana na simulizi la nabii Mikaya kuhusu manabii wa kweli wa Mungu na manabii wa uwongo? 1 Wafalme 22:1-17,24-28
2. BWANA aliwaonaje manabii wa uwongo katika siku za nabii Yereimia? Yereimia 14:14-15
3. Yesu alitoa unabii gani kuhusu manabii wa uwongo? Mathayo 24:24, 7:15
4. Tunawezaje kutofautisha kati ya manabii wa kweli wa Mungu na manabii wa uwongo? Mathayo 7:16-20,21-23, Isaya 8:20, n.k.